



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA  
SHIRIKA LA VIWANGO TANZANIA



ISO 9001:2015 Certified

Mwanachama wa Shirika la Viwango la Kimataifa (ISO), Codex Alimentarius Commission (WHO/FAO) na Wakala wa ISO na Mashirika ya Viwango ya Mataifa mbalimbali

TAARIFA KWA UMMA KUHUSU MATUMIZI YA KEMIKALI KATIKA UIVISHAJI WA NDIZI

Dar es Salaam, 13 Oktoba, 2024

Hivi karibuni, kumekuwepo na taarifa inayosambaa kwenye mitandao ya kijamii inayoelezea matumizi ya kemikali kwa ajili ya kuivisha ndizi katika Jiji la Dar es Salaam na kutilia mashaka usalama wa afya ya mlaji wa bidhaa husika.

Shirika la Viwango Tanzania (TBS) baada ya kupata taarifa hiyo limefanya ukaguzi na uchunguzi wa awali katika maeneo/ masoko mbalimbali Jijini Dar es Salaam ambapo zoezi la kuivisha ndizi hufanyika na kugundua wafanyabiashara wanatumia gesi maalum (ethylene) kuivisha matunda hayo.

TBS inapenda kuufahamisha umma kuwa teknolojia inayotumika kuivisha matunda kwa kutumia kemikali ya *ethylene* ni utaratibu wa kawaida unaotumika duniani kote na hauna madhara yoyote kiafya. Aidha, kemikali inayotumika ya *ethylene* imefanyiwa uchunguzi wa kitaalam juu ya usalama wake na inaruhusiwa kwa matumizi hayo ya kuivisha matunda.

Hivyo, teknolojia hii imepunguza kwa kiasi kikubwa hasara iliyokuwa inajitokeza wakati wa usafirishaji wa matunda yalioiva kwani imewezesha wafanyabiashara kununua/ kusafirisha matunda yaliyokomaa na kuyaivisha kwa wakati mmoja, na kwa kiwango sawa, na pia kufanya ndizi hizo kutoharibika katika kipindi cha muda mrefu zaidi, ikilinganishwa na zile zilizoivishwa kwa njia ya asili ambayo matunda hutoa gesi asilia ya *ethylene* ili kuiva.

TBS inapenda kuuhakikishia umma kuwa inaendelea kulinda usalama na ubora wa bidhaa zote wakati wote

Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kupitia kituo cha huduma kwa wateja kwa namba hiyo **0800110827**.

Imetolewa na:

Gladness H. Kaseka  
**MENEJA UHUSIANO NA MASOKO**

**TBS MAKAO MAKUU**

Shirika la Viwango Tanzania  
Barabara ya Sam Nujoma /  
Morogoro, Ubungo, Dar es Salaam  
S. L. P. 9524  
DAR ES SALAAM, TANZANIA  
Simu Na: +255 22 245 0298/  
+255 22 245 0206  
Nukushi: +255 22 2450959  
Namba ya Simu Bila Malipo: 0800110827  
Barua pepe: info@tbs.go.tz  
Tovuti: http://www.tbs.go.tz  
Barua pepe kwa ajili ya malalamiko ya  
wateja: malalamiko@tbs.go.tz  
Twitter: TBS\_Tanzania  
Instagram: tbs\_Viwango

**TBS KANDA YA  
KATI**

Jengo la Kambarage  
S. L. P. 2956  
DODOMA,  
TANZANIA  
Simu Na:  
+255 26 2520310

**TBS KANDA YA  
ZIWA**

Jengo la NSSF,  
Ghorofa ya 3  
S. L. P. 1814  
MWANZA,  
TANZANIA  
Simu Na:  
+255 28 2505044

**TBS KANDA YA  
KASKAZINI**

Jengo la NSSF (Mafao  
House), Ghorofa ya 2  
S. L. P. 2399  
ARUSHA,  
TANZANIA  
Simu Na:  
+255 27 2520143

**TBS KANDA YA  
NYANDA ZA JUU  
KUSINI**

Jengo la NHIF,  
Ghorofa ya 7  
S. L. P. 1674  
MBEYA, TANZANIA  
Simu Na:  
+255 25 2502848

**TBS KANDA YA  
KUSINI**

Jengo la MTUWASA  
S. L. P. 1396  
MTWARA,  
TANZANIA  
Simu Na:  
+255 23 2334477

**TBS KANDA YA  
MAGHARIBI**

Jengo la NSSF (Mafao  
House), Ghorofa ya 2  
S. L. P. 1276  
KIGOMA,  
TANZANIA  
Simu Na:  
+255 28 2804023